



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA TANGA**



(Imeanzishwa chini ya Sheria ya Huduma za Maji ya Mwaka 1997 Kupitia Agizo la Huduma za Maji (Tamko la Eneo la Huduma) la mwaka 1998 lililotolewa kupidia Gazeti la Serikali Na. 61 la tarehe 13.02.1998)

Tangazo hili limeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)

TANGAZO KWA UMMA

MATOKEO YA MAUZO YA HATIFUNGANI YA KIJANI YA MIUNDOMBINU YA MAJI TANGA

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) inatoa taarifa kwa umma kuwa mnamo tarehe 20 Februari 2024, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania, ilitao idhini kwa Tanga UWASA kuuza Hatifungani ya Kijani ya miaka 10 yenye thamani ya shilingi bilioni 53.12 kwa ajili ya kupata fedha za kuboresha miundombinu ya usambazaji wa maji na utunzaji wa mazingira.

MATOKEO YA MAUZO YA HATIFUNGANI

Mauzo ya hatifungani ya Tanga UWASA yalifunguliwa tarehe 22 Februari 2024 na kufungwa tarehe 4 Aprili 2024, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 54.72 kimepatikana ikilinganishwa na shilingi bilioni 53.12 zilizotarajiwa kukusanya, sawa na mafanikio ya asilimia 103.

MUHTASARI WA HATIFUNGANI YA KIJANI YA MAJI TANGA

Muhtasari wa takwimu muhimu za mauzo ni kama ifuatavyo:

Mtoaji	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA)
Maeleo na Aina ya Hatifungani	Isiyo kuwa na dhamana
Jina la Hatifungani	Hatifungani ya Kijani ya Miundombinu ya Maji Tanga
Muda	Miaka 10
Tarehe ya Toleo	30 Aprili 2024
Jumla ya Kiwango kilichotolewa	TSH 53,120,000,000
Jumla ya kiasi kilichokusanya	TSH 54,723,600,000.00
Kiwango cha matokeo	103%
Jumla ya kiasi kilichokubaliwa	TSH 53,120,000,000
Riba inayotarajiwa	13.5% kwa mwaka, itakayolipwa kila baada ya miezi sita.
Bei ya Hatifungani	Ni ile iliyo tangazwa
Kiwango cha chini	TSH 500,000 (na nyongeza ya mafungu ya 10,000)
Matumizi ya fedha zilizopatikana	Fedha zilizopatikana zitatumika kutekeleza shughuli za kuboresha miundombinu ya usambazaji wa maji na utunzaji wa mazingira jijini Tanga kama ilivyoainishwa kwenye kifungu namba 2.1 cha Muundo wa Hatifungani hii.

SERA YA UGAWAJI

Kutokana na mafanikio ya usajili ya 103%, Tanga UWASA imepata idhini ya CMSA ya:

- Kupokea maombi ya jumla ya TSH 53,120,000,000 tu ambayo ni kiasi kilichoidhinishwa kwenye Waraka wa Matarajio wa Hatifungani.
- Kurejesha kiasi cha TSH 1,603,600,000.
- Kukubali maombi yote sahihi yaliyopokelewa kutoka kwa wawekezaji wote kwa asilimia mia moja (100%) ya maombi yao kwa mujibu wa Sera ya Ugawaji, isipokuwa Mshauri Kiongozi wa Tanga UWASA).

MAELEZO ZAIDI

Endapo mwombaji wa Hatifungani atahitaji ufanuzi, anashauriwa kuwasiliana na Wakala wa Soko la Hisa au NBC kuititia NBC_CustodialServices@Nbc.co.tz au +255 768 980 076.

TAREHE ZA MATUKIO MUHIMU

Tafadhalii angalia tarehe zilizopendekezwa kufuatia ufungaji wa mauzo ya hatifungani:

Maelezo	Tarehe
Tarehe ya kutaarifiwa (kupitia baruapepe / simu)	Jumanne 30 Aprili 2024
Tarehe ya Toleo	Jumanne 30 Aprili 2024
Tarehe ya Kuiva kwa Hatifungani	Ijumaa 28 Aprili 2034
Tarehe ya kuweka katika akaunti ya CDS	Jumanne 30 Aprili 2024
Tarehe ya Malipo ya Riba	30 Oktoba, 30 Aprili
Tarehe ya kuorodhesha hatifungani kwenye soko la hisa	Jumatano 8 Mei 2024

SHUKRANI

Uongozi wa Tanga UWASA unatoa shukrani za dhati kwa taasisi zote zilizofanikisha uuzwaji wa hatifungani ya Tanga UWASA. Taasisi hizi ni pamoja na Bodi na Uongozi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA); Bodi na Uongozi wa Soko la Hisa la Dar Es Salaam (DSE); Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji ya Maendeleo (UNCDF); Taasisi ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha Barani Afrika (FSD Africa) ; Mshauri Kiongozi wa Tanga UWASA, NBC Bank; Dalali Mfadhilli wa Tanga UWASA, Vertex International Securities Limited; Washauri wa Masuala ya Kisheria, Anjarwalla & Khanna Tanzania; Washauri wa Masuala ya Kifedha, FIMCO Limited; Wakaguzi na Watoa Taarifa za Mahesabu, INNOVEX Auditors; na kampuni ya ISS Corporate Solutions, iliyotoa Ithibati kwenye Muundo wa Hatifungani ya Tanga UWASA.

Imetolewa na:

Mkurugenzi Mtendaji
Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga,
S.L.P 5011,
21103 Tanga, Tanzania

Tarehe: 30 Aprili 2024

Tangazo hili limetolewa kwa idhini ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa mujibu wa kanuni za Mamlaka za Matangazo, G.N. Namba. 15 ya mwaka 1997.

